05:59

# Mwito wa Kutuma Maombi ya Mpango wa Wabunifu

Tuma kupitia mediainnovationnetwork.org

+254 780 993 137

Makataa

31 Agosti 2021



Kuna

## $20,000

za kupiga jeki timu 9

akumediafutures

Media Innovation Centre

Kituo cha Ubunifu wa Tasnia ya Uanahabari cha Chuo Kikuu cha Aga Khan wanatoa ruzuku ya $20,000 ili kuongeza chachu katika makampuni ya uanahabari yaliyo vijijini na mjini kutoka Kenya, Uganda na Tanzania.

THE AGA KHAN UNIVERSITY
*Graduate School of Media and Communications*

DW Akademie

MEDIA CHALLENGE INITIATIVE

Tanzania Media Foundation

KFW
Bank aus Verantwortung

german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

# Pogramu ya Innovators-in-Residence 2021-2022

## Media Innovation Center
## The Aga Khan University
## (Graduate School of Media and Communications)

### Kielezo cha Hisia.

Kituo cha AKU GSMC Media Innovation Centre, kwa ushirikiano na DW Akademie, Media Challenge Initiative wanatafuta wabunifu katika tasnia ya uanahabari kutoka Kenya, Uganda na Tanzania watakaojiunga kwenye programu ya Innovators-in-Residence ya mwaka 2021-2022, programu inayoendeshwa kwa kipindi cha miezi 12 ya kukuza na kuchochea ubinifu kupitia ushauri, mafunzo kwa wabunifu katika tasnia ya uanahabari kanda ya Afrika Mashariki.

Lengo letu ni kuhakikisha kwamba wabunifu kutoka maeneo ya vijijini na mjini wanapata fursa ya kujiunga na programu hii na ndio maana, kutakuwa na **mpango maalum mahususi kwa ajili ya wabunifu wa kutoka vijijini** katika timu itakayoshiriki mwaka huu.

Tunataka kusaidia **wabunifu wanaotafuta mbinu za kukuza uanahabari maeneo ya vijijini** nchini Tanzania, Uganda na Kenya. Hususan, wabunifu wenye miradi inayowafikishia wananchi habari, kuhimiza mijadala ya wazi sambamba na kuimarisha kushirikishwa kwa jamii za vijijini ikizingatiwa changamoto za uwepo wa lugha mbalimbali, upatikanaji mdogo wa mtandao wa intaneti, upatikanaji mdogo wa habari kutoka kwa vyombo vikubwa vya habari na viwango vya chini vya elimu. Wabunifu wanaoendesha shughuli zao nje ya miji kama Nairobi, Dar es Salaam na Kampala wanahimizwa sana kutuma maombi.

**Wabunifu kutoka maeneo ya miji wanahimizwa pia watume maombi** akwa sabau tumetenga nafasi zao pia.

Timu **9** zitakazoibuka washindi, **timu 4 kutoka Uganda, 4 kutoka Tanzania na moja kutoka Kenya** watajiunga nasi kwa kipindi cha miezi 12 na watafaidi mambo yafuatayo ili kufanikisha uzalishaji wa bidhaa zao.

- Ofisi ya kuendeleza ubunifu wako nchini mwako na kukutanishwa na mtandao wa mashirika na watu yenye ushawishi mkubwa katika tasnia ya uanahabari.
- Mafunzo na ushauri wa kitaalamu kulingana na mahitaji ya wabunifu sambamba na mafunzo ya viwango vya juu kutoka kwa wataalamu wenye weledi na uzoefu katika tasnia ya habari na biashara.
- Kuwa mwanachama wa kudumu wa jumuiya yetu ambayo bado ipo hatua za awali ya wabunifu wa uanahabari na vyombo vya habari.
- Malipo ya kila mwezi ya $1,000 kwa kila muhula.
- Udhamini wa ruzuku ya hadi $20,000.

Tunahimiza sana waombaji watume maombi **kama timu** za wanahabari, waandishi, wasanii wa picha, wachanganuzi wa data, wapiga picha, wapiga picha za video, wasanifu michoro, wachora vibonzo, wachoraji, watengeza programu za simu (app), wataalamu wa programu za kompyuta na/au wahuishaji ambao watafanya kazi kama timu kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazokabili tasnia ya uanahabari katika kanda ya Afrika Mashariki. **Tunapokea maombi ya watu binafsi,** lakini wawe tayari kuunda timu mara tu watakapofuzu kujiunga na programu hii.

- **Uanahabari katika jamii au unaolenga jamii fulani:** Vyombo vya habari katika jamii (makampuni ya redio na tovuti za habari) zinazoshughulikia masuala muhimu katika jamii za mashinani. Wanahabari wanaofanya kazi katika maeneo ya vijijini nchini Kenya, Uganda, na Tanzania wanahimizwa kutuma maombi. Tunapenda kusaidia miradi inayotusaidia kupata majibu ya swali hili: **Jinsi gani tunaweza kubadilisha uanahabari katika ngazi ya jamii ili ukidhi mahitaji ya jamii lengwa?**
- **Uanahabari unaolenga vijana:** Miradi ya ubunifu na mashirika ya teknolojia yanayozalisha au yanayodhamiria kuzalisha maudhui ya yanayolenga vijana. Miradi ya ubunifu inayotafuta muafaka wa changamoto zinazowakabili vijana Afrika Mashariki sambamba na kuweka maudhui haya katika muundo wa dijitali unaoendana na mahitaji ya vijana. Katika kitengo hiki tunapenda kujibu swali lifuatalo: **Ni njia gani tunaweza kushirikisha hadhira ya vijana wadogo?**
- **Kutambua ukweli:** Ubunifu utakaosaidia wanahabari na waandishi kutatua changamoto za habari za uongo na upotishaji katika kanda ya Afrika Mashariki. Tuko tayari kupokea miradi inayojibu swali lifuatalo: **Ni njia gani tunazoweza kutumia kukabiliana habari za uongo na upotoshaji?**
- **Uanahabari wa dijitali:** Ubunifu unaoweka msukumo mkubwa katika kutoa huduma za uanahabari wa viwango vya juu kwa kutumia teknolojia iliyopo kutuma maudhui kidijitali kama vile picha, matangazo ya sauti, video na miundo mingine ya kuonekana kwa macho ya kutoa maudhui ya kuhabarisha. Katika kitengo hiki, tunatafuta miradi ya ubunifu itkayojibu swali lifuatalo: **Ni kwa namna gani tunaweza kutumia zana na mbinu za teknolojia iliyopo kuhabarisha kwa namna yenye kuleta tija?**
- **Masimulizi au 'uanahabari mbadala':** Ubunifu unaoweka msukumo mkubwa katika kusimulia uanahabari tena katika njia ambazo si za kawaida kama vile masimulizi, vipindi vya masimulizi na tamthilia fupi. Tunapenda kujua: **Ni njia gani zinaweza kutumiwa kuhabarisha kwa namna ambayo inahusisha na kuhimiza hadhira kutafakari kuhusu habari husika?**

## Sifa za Mwombaji?

- Wabunifu katika tasnia ya uanahabari kutoka Kenya, Uganda na Tanzania. Wanahabari na wabunifu wanaofanya kazi maeneo ya vijijini **wanahimizwa sana kutuma maombi**.
- Wabunifu wanaofanya kazi katika timu ambazo zimeundwa tayar au **wabunifu binafsi wanaotuma maombi lakini wako tayari kuunda timu kwa ajili ya programu hii**.

- Tunakubali maombi ya wabunifu wenye miradi inayochapisha maudhui kwa lugha yoyote inayotumika Afrika Mashariki. Maombi yatumwe kwa lugha ya Kiingereza.
- Tunakubali maombi ya ubunifu unaotafuta muafaka wa changamoto zinazokabili tasnia ya uanahabari na vyombo vya habari mbali na usimulizi. Pia tunakaribisha maombi ya programu za simu (App) na miradi inayowasaidia wanahabari kutetekeleza majukumu yao kazini.
- Projects that address journalism and media challenges other than storytelling are welcome. Apps and projects that support journalists and existing media houses in their work are invited to apply.
- Washiriki lazima wawe na umri usiopungua miaka 18.

## Jinsi ya Kutuma Maombi

Tunatambua changamoto zinazoweza kuwapata waombaji wakati wa kutuma maombi mtandaoni, kwa hiyo tumeweka njia kadhaa za kutuma maombi yako:

1. **Maombi ya mtandaoni:** Ikiwa una intaneti ya uhakika, tafadhali tumamaombi yako kwenye fomu ya google inayopatikana

   PATA FOMU HAPA

2. **Maombi ya nje ya mtandao:** Ikiwa huna intaneti, tafadhali tumia mojawapo ya njia zifuatazo:

### Njia ya A

Tuma maombi yako kupitia huduma yaWhatsApp kwenda namba yetu ya simu. Ikiwa utachagua njia hii, WhatsApp, tuma ujumbe au upige simu kwenda namba hizi za simu +254780993137 na utatumiwa fomu ya maombi mara moja. Hakikisha unajibu maswali ya utakayoulizwa kabla ya siku ya mwisho.

Pia unaweza kutuma maombi yako katika ofisi zetu. Ikiwa unataka kutumia njia hii ya kutuma maombi, tafadhali chukua fomu za maombi kutoka kwa ofisi zetu na uhakikishe unarudisha fomu za maombi baada ya kujaza kabla ya siku ya mwisho ya kupokea maombi.

**Media Innovation Centre,**
**Ghorofa ya 2,**
**06 Peponi Road, Westlands, Nairobi, Kenya.**

RAMANI

### Njia ya B

You could visit our offices in Nairobi Kampala and Dar es Salaam and you will be provided with an internet connected computer to make your application online. Please notify the respective hub at least a day before for ease of access. See details of our offices and partner hubs below.

### Njia ya C

Tuma maombi yako kupitia kwa washirika wetu. Kama utachagua njia hii, tafadhali hakikisha unachukua fomu za maombi kutoka kwa ofisi za washirika wetu na uhakikishe unairudisha baada ya kuijaza kabla ya tarehe ya mwisho.

- **Waombaji kutoka Uganda,** unaweza kuchukua na kurudisha fomu yako ya maombi katika ofisi za washirika wafuatao:

  i. The Innovation Village (Jinja)
  The Innovation Village Jinja
  Plot 5 Main Street, Jinja
  Opposite Local Flavours and DHL.

  ii. Northern Uganda Media Club (NUMEC) in Gulu,
  Northern Uganda Media Club,
  P. o Box 126
  Upper Churchill Drive
  Gulu City, Uganda

  iii. Media Challenges Initiative (MCI) in Kampala
  MCI Media Hub
  Roof Top, Tirupati Mall,
  Kabalagala, Kampala
  +256775434172/ +256705807674

  iv. Aga Khan University, Kampala
  Aga Khan University
  Plot 9/11, Colonel Muammar Gaddafi Road
  P. O. Box 8842
  Kampala, Uganda
  Tel: +256 414 349 494

- **Kwa waombaji kutoka Tanzania,** unaweza kuchukua na kurudisha fomu yako ya maombi katika ofisi za washirika wafuatao:

  i. Ennovate Hub in Mwanza.
  Flat 5&6, Second Floor,
  Academic Block,
  St Augustine's University of Tanzania, Malimbe, Mwanza.

  ii. Tanzania Media Foundation in Dar-es-Salaam
  Tanzania Media Foundation,
  No. 2, Plot 18
  Dahomey Street, Kinondoni, next to the Leaders grounds.

  iii. The Aga Khan University offices
  Salama House
  Urambo Street

Tarehe ya mwisho ya kutuma maombi ni **Jumanne ya Tarehe 31 Agosti 2021.**

## Warsha za Awali.

Kwa wanaotaka kushiriki programu hii, kutakuwa na warsha za ana kwa ana kuhusu Mwongozo wa Kuwasilisha Pendekezo ili kupiga msasa ubunifu wako. Zifuatazo ni taarifa za warsha hizo.

17:59

Pogramu ya Innovators-in-Residence 2021-2022

## Warsha za Mtandaoni

**Tarehe:** 23 Julai
**Mada:** Human Centered Design and Pitching
**Mahali:** Mtandaoni/ zoom

TUMA MAOMBI HAPA

## Warsha za Ana kwa Ana

**Tarehe:** 11-12 Agosti
**Mada:** Human Centered Design and Pitching
**Mahali:** Ennovate Hub (Mwanza)
Tuma maombi yako kwa kupigia simu Ennovate Hub kupitia +255 752 817 723

**Ukitakata kuona miradi ambayo tumewahi kudhamini na kusaidia, angalia timu yetu ya sasa; ONA Stories kutoka Tanzania, Minority Africa kutoka Uganda, na Lam Sisterhood kutoka Kenya**

**Waombaji wataorodheshwa na kusailiwa na kamati ya uteuzi na jopo la wataalamu wanaojisimamia.**

## Kuhusu:

**Kituo cha Media Innovation Centre- cha Chuo Kikuu cha Aga Khan University,** kwa ushirikiano na washirika wa mradi huu, Deutsche Welle (DW) Akademie, Wakfu wa Vyombo vya Habari Tanzania (Tanzania Media Foundation - TMF), na Media Challenge Initiative (MCI) nchini Uganda husaidia vizazi vya wabunifu wa baadaye kutafuta muafaka wa changamoto mtambuka zinazokabili tasnia ya uanahabari kupitia ubunifu wao.

**Kituo cha Media Innovation Centre** kinadhaminiwa na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani ((KfW Entwicklungsbank) chini ya mwavuli wa mradi wa Media Futures East Africa (MFEA). Shabaha kuu ya MFEA ni kuimarisha na kujenga vyombo vya habari endelevu vyenye viwango Afrika Mashariki, ili kuleta mchango chanya katika ubora na upatikani wa vyombo vya habari Afrika Mashariki.

**DW Akademie ni kitengo cha Deutsche Welle**. Kama mshirika wa kimkakati wa Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi ya Ujerumani, DW Akademie inatekeleza miradi ya kuendeleza vyombo vya habari inayolindaa haki ya binadamu ya uhuru wa mawazo na kukuza upatikanaji wa habari bila malipo. Wanasaidia watu binafsi kutoa maoni yao kwa kuzingatia taarifa za ukweli na sahihi sambamba na kuhimiza watu kushiriki mijadala inayohusu masuala ya umma na kutetea maoni yao. Huu ni mchango muhimu wenye kuleta ufanisi katika kuchochea maendeleo yenye tija katika jamii zao na kuboresha maisha yao.

**Shirika la Media Challenge Initiative** ni shirika lisilo la serikali lenye ofisi zake jijini Kampala, Uganda ambalo limejitolea kuandaa wanahabari wa kizazi cha kesho nchini Uganda na Afrika ambao wana ujuzi wa kutumia maarifa yao katika kufanikisha uanahabari unaotatua matatizo ya jamii. Dira ya MCI ni kuwa na kizazi cha wanahabari kilichojengewa uwezo wa kuleta maendeleo na mabadiliko chanya na katika jamii kupitia tasnia ya uanahabari.




THE AGA KHAN UNIVERSITY
*Graduate School of Media and Communications*

DW Akademie

MEDIA CHALLENGE INITIATIVE

Tanzania Media Foundation

KFW
Bank aus Verantwortung

german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT